kukataa, na kukataa neema hii wakati wowote wa maisha yake. Wengi wanafundisha, "ukiokolewa, daima umeokolewa"; mafundisho hayo hayana msingi katika Neno la Elohim. Mwanadamu anapotubu dhambi na kumgeukia Elohim hapotezi uhuru wake wa kuchagua. Bado tuna haki na uwezo wa kuamua hatima yetu wenyewe.

**Somo la Maandiko: 2 Petro 2.**
**Fungu la Kukariri: Yuda 24, 25.**

1. Je, inawezekana kujiweka nje ya kundi la Elohim? Waebrania 12:15-17.
2. Ni ukweli gani wa kusikitisha ambao Masihi alisema wakati mmoja? Mathayo 24:12.
3. Je, tuna uhakikisho gani mtukufu? Mathayo 24:13.
4. Jinsi gani Paulo alionyesha uwezekano wa kuanguka? 1 Wakorintho 9:27.
5. Baada ya kupata imani nini kinaweza kutokea? Luka 22:32; 1 Timotheo 1:19, 4:1; 5:8, 12; 2Timotheo 2:16-18.
6. Hii ikiwa ndivyo ilivyo, tunapaswa kujihusisha vipi na Injili? 1 Wakorintho 15:58.
7. Ikiwa mtu ataanguka kutoka kwa neema na kubakia hivyo kwa makusudi, ni nini kilichosemwa juu ya hatima yake? 2 Petro 2:20-22.



Mwokozi alivyosema itakuwa kabla ya kurudi Kwake.

5. Wajibu wetu ni nini katika wakati huu wa giza wa sasa? Isaya 60:1,2.
6. Je! Ni nini kitafanywa kwa wale wasiozaa matunda katika kazi ya Bwana? Yohana 15:2, na Mathayo 25:30.
7. Je, watenda kazi kwa ajili ya Masihi wanapaswa kuvikwa nini? Waefeso 6:10-18.

**Maelezo**. "Si kwa nguvu wala si kwa uwezo, bali ni kwa Roho Yangu," Zek. 4:6, kwamba kazi yenye mafanikio inatimizwa katika shamba la mizabibu la Bwana. Ni maisha ya maombi, na kuwekwa wakfu kamili kunategemea kabisa Roho na nguvu kutoka juu, kuongoza, na kushawishi mioyo ya watu. "Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho"

8. Je! Wazazi wameagizwa kuwafundisha watoto wao nini? Kumbukumbu la Torati 6:6,7.
9. Je, tunachukuliwa kuwa wa familia moja na malaika wa mbinguni? Waefeso 3:14,15. Ufunuo 22:8,9.

**Maelezo**. Kutokana na andiko hili, tunaona halizungumzii familia katika wingi, bali familia moja tu, ambayo malaika ni sehemu yake. Wana nguvu zaidi, hata hivyo wageni hawa wasioonekana na wajumbe hupiga kambi



3. Wataendelea kulala katika mavumbi ya nchi mpaka lini? Ayubu 14:10-12; 1 Wakorintho 15:42-58.
4. Je! Ayubu alisema atasubiri nini? Ayubu 14:14.
5. Je! Atasubiri mabadiliko haya akiwa wapi? Ayubu 17:13.
6. Je! Mfalme Hezekia aliandika nini kuhusu kifo na kaburi? Isaya 38:18, 19; Zaburi 30:9.
7. Ni nini imelezewa kuhusu mawazo ya wale waliokufa? Zaburi 146:4; Mhubiri 9:5, 6, 10.
8. Je, wafu wanaweza kumsifu Bwana? Zaburi 115:17.
9. Je, kuna ukumbusho katika mauti na kaburini? Zaburi 6:5.
10. Je! Ni nini kilichosemwa tena juu ya wale waliokufa katika Bwana? Ufunuo 20:6.

*******************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Pili
2023

Ya
Aprili, Mei, Juni.
**(Nisan, Iyar, Sivan, Tamuz)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

kuwazunguka waaminifu. Waaminifu wanategemea kikamilifu mkono wa usaidizi kutoka juu kuwaongoza, na kuwaelekeza na kuwalinda.

10. Ni ahadi gani nzuri ambayo Bwana ametoa kwamba juhudi na dhabihu zetu hazitakuwa bure, tunapofanya kazi kwa ajili ya waliopotea? Isaya 55:10,11.
11. Je! Bwana anapenda mtoaji wa aina gani? 2 Wakorintho 9:6-15.
12. Je! Ni maswali gani ambayo tunayoamriwa tuepuke, na kwa nini? 2 Timotheo 2:23-25.

*******************************

**Somo la Aprili 22, 2023 (Iyar 1, 5783)**

## MKUU MIONGONI MWENU NI MTUMISHI

**Somo Kuu: Luka 9:46-62.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 20:27.**

1. Ni ugomvi upi uliotokea miongoni mwa Mitume katika Luka 22:24?
2. Mwokozi alikuwa wa kuhudumiwa au nikuwahudumia wengine? Luka 22:27.
3. Mwokozi alisema nini kuhusu viongozi wa Mataifa kutawala kwa nguvu na kuonyesha mamlaka yao? Marko 10:42.



3. Je! Ni ufanisi gani mzuri utatokea kutokana na mazoezi haya? Mstari wa 4, 5.
4. Yahshua alijitukuza Mwenyewe kwa njia yoyote? Mstari wa 8.
5. Je! Ni nini kilichofuatia unyenyekevu Wake mkubwa? Mstari 9-11.
6. Ikiwa tunaweza kuwa na hatia katika uhusiano wetu sisi wenyewe, ni nini kitakachotokea katika hali zetu? Mstari wa 14, 15.
7. Ni hali gani nzuri iliyokuwapo kati ya ndugu katika siku za Paulo? Mstari wa 18-20.
8. Je, ni mashauri gani sawa yanayopatikana katika Wakolosai 3: 11-17?
9. Wakati Masihi anakaa ndani yetu katika Roho Mtakatifu, ni nini itakuwa matokeo siku zote? Yohana 15:4, 5.
10. Ikiwa hatutajitolea kushinda nafsi za watu kwa ajili ya Ufalme wa Elohim, matokeo yatakuwa yapi? Mstari wa 6.
11. Je, kushinda nafsi za watu itaongeza uwezo wetu tukiwa na Elohim kwa sala iliyojibiwa? Mstari wa 7, 8, 16.

*******************************

**Somo la Mei 27, 2023 (Sivan 7, 5783)**

## USHIRIKA WA WAKATI WOTE NA ELOHIM

**Maelezo**. Ingawa ni kweli kwamba neema ya Elohim daima hupanuliwa ili kumwinua mwenye dhambi kutoka kwa dhambi, ni kweli pia kwamba mtu anaweza



**Somo la Aprili 1, 2023 (Nisan 10, 5783)**

## UTIIFU WA MASIHI KWA ELOHIM – KUTESEKA KWA MASIHI KWA AJILI YA WOKOVU WETU

**Somo Kuu: Isaya 53.**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 2: 9, 10.**

1. Masihi anafananishwa na nini katika kukua kwake? Isaya 53: 2.
2. Je, watu waliokwenda katika giza waliona nini? Isaya 9: 2.
3. Je, ni asili gani Yahshua alijichukulia mwenyewe wakati alikuja duniani kuwakomboa watu wake? Waebrania 2:16.
4. Alitaka kufanywa kama nani? Mstari wa 17, 18.
5. Kwa nini aliitwa Yahshua? Mathayo 1:21.
6. Ni jina gani lingine alijipea mwenyewe? Yohana 10:11.
7. Kwa nini Masihi alikuja ulimwenguni? 1 Timotheo 1:15.
8. Je, upendo wa Elohim kwa ulimwengu ulikuwa mkubwa kiasi gani? Yohana 3:16.
9. Je, ni zawadi gani nzuri MMasihi hupata kutoka kwa Elohim kupitia Masihi? Warumi 6:23 (sehemu ya mwisho).



8. Ni kwa ajili ya sala ya nani alisaidiwa? Mstari wa 5.
9. Inawezekanaje kwa maombi yetu kujibiwa kwa haraka? Dan. 9:21.
10. Ni uhusiano gani muhimu kati ya mwanadamu na malaika, unaohusu kuelewa maandiko? Mstari wa 22.
11. Tutawezaje kupata msaada wa Elohim? Mathayo. 7: 7, 8.
12. Katika uchungu wa Gethsemane, Elohim alimsaidiaje Yahshua katika wakati huu wa mgogoro? Luka 22:43.
13. Je malaika wa Mbinguni wanayo maslahi kwa mwanadamu? Luka 15; 10.
14. Katika wakati wa shida kubwa ni nani ambaye atakuwa mlinzi wetu? Zab. 91.8, 10, 11.

*******************************

**Somo la Juni 24, 2023 (Tamuz 5, 5783)**

## BAADA YA KUFA, NI NINI?

**Somo Kuu: 1 Wathesalonike 4.**
**Fungu la Kukariri: 1 Wathesalonike 4:16.**

1. Je! Biblia inasema kifo ni nini? 1 Wathesalonike 4:13, 14.
   **Maelezo**. Wakati mtu amelala anapoteza fahamu kabisa; muda unaendelea bila kupimwa, na kazi ya ufahamu wa akili inasimamishwa kwa muda.
2. Wafu wanalala wapi? Danieli 12:2.

11. Alionyeshaje neema kwa siku za kale, za sasa, na za baadaye? 2 Wakor.1:10.
12. Katika kumkubali Masihi ni nini kinachowezekana kujua? Matendo 13:38, 39.

*******************************

**Somo la Mei 20, 2023 (Iyar 29, 5783)**

## NGUVU ZA ELOHIM KUPITIA ROHO MTAKATIFU

**Somo Kuu: Wafilipi 2: 1-28.**
**Fungu La Kukariri: Wafilipi 2:15.**

**Maelezo**. Sura hii ambayo ni nzuri inatufundisha jinsi ya kushirikiana na wengine katika umoja wa kweli na furaha. Tafakari maneno haya: "Ikiwa kuna faraja yoyote katika Masihi, ikiwa faraja ya upendo, ikiwa ushirika wa Roho", nk.

1. Je! Ni mambo gani manne ambayo ni muhimu ili kufikia umoja huu kama ulivyotolewa kwa Wafilipi. 2:2?
2. Badala ya kufanya kazi kupitia ugomvi na utukufu usiofaa, tunapaswa kufanya kazi zetu aje? Mstari wa 3.
   **Maelezo**. Maneno haya ni mazuri sana, "kwa hali ya unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake."Ikiwa tutafuata ushauri huu ambao ni bora, hakuwezi kuwa na ugomvi. Unawezaje (ugomvi) kuwepo?



4. Je, alipendekeza hilo jambo au alililaani miongoni mwa viongozi wa Kanisa? Marko 10:43.
5. Mwokozi alitupea mfano wa kuhudumiwa, au kuwahudumia wengine? Marko 10:44, 45.
6. Je, aliwaamuru viongozi na watu wengine wamfuate Yeye, na kuzifuata nyayo zake? Yohana 8:12; 1 Petro 2:21.
7. Ni amri zipi zaidi ambazo zimepeanwa kwa wazee na viongozi kuhusu kulazimisha na uongozi wa nguvu na kwa njia ya kutia watu uoga? 1 Petro 5:1-3.
8. Je, ni nafasi na wajibu upi kwa viongozi katika ulezi wa Kanisa la Elohim? Matendo 20: 28.
9. Ni nini itakuwa kazi ya kila mwanafunzi (mfuasi) wa Masihi kuthibitisha upendo wake kwa ajili yake? Yohana 21:15.

   **Maelezo**: Maneno ya kila mwanafunzi wa kweli yatakuwa yameimarika kwa chakula cha kutia nguvu ili kuweza kukaza mwendo. Pia ataweza kuuondoa ubinafsi kwa njia ya kujikana na kuwapendelea wengine badala yake mwenyewe.
10. Ili kulivutia jukumu hili takatifu juu yetu, Mwokozi wetu alitumia maneno "Kulisha kondoo wangu"; maneno haya yalirudiwa kwa Petro? Yohana 21:16, 17.
11. Je, maisha ya Paulo yalikuwa yamejaa kujikana na dhiki, au yeye (kwa sababu alikuwa kiongozi



11. Je, Mtume Yohana alipata fursa ya kuona jiji hili la mbinguni? Ufunuo 3:12; Ufunuo 21: 1, 2, 10.
12. Ili kuingia mji huu mtakatifu, pasipoti yetu inafaa kuwa nini? Ufunuo 22:14; Mathayo 19:16, 17.

*******************************

**Somo la Juni 17, 2023 (Sivan 28, 5783)**

## JE, KUNA MALAIKA NA NI KWA NINI?

**Somo Kuu: Waebrania. Sura ya 1.**
**Fungu La Kukariri: Wae. 1:14.**

1. Je, ni uumbaji gani mwingine wa viumbe ambao ni sawa na mwanadamu, na hali yetu ni gani ikilinganishwa nao? Zab. 8: 4, 5.
2. Kusudi lao na kazi yao katika uumbaji ni nini? Zab. 34: 7; Heb. 1:13, 14.
3. Je! Muumba wetu anazingatia mtu kuwa wa familia sawa na malaika? Waefeso. 3:14, 15; Ufu. 22: 9.
4. Je, familia hii ina jina sawa, na jina lake ni lipi? Waefeso. 3:14, 15.
5. Je, ni nini kilichosemwa juu ya malaika wa Mbinguni kuhusu Amri Takatifu? Zab. 103: 20.
6. Ni kwa njia gani hawa wajumbe wa mbinguni wanatumwa kuwa msaada wetu? Mathayo. 26:53.
7. Petro alifungwa gerezani na minyororo miwili, alifunguliwaje? Matendo 12: 7-10.



10. Ni nguvu gani iliyotolewa juu ya dhabihu yake kwa ajili ya watu wake mwenyewe? Ilipeanwa kupitia nani? Yohana 10:17, 18.
11. Je, mateso ya Masihi yalikuwa mengi na tofauti? Isaya 53: 8-10.
12. Je! Ni nani alifanya kaburi pamoja naye? Mstari wa 9.

   **Maelezo**. - Masihi, mfano wetu mkuu, aliendaakitenda mema, na akateseka sana kwa ajili yetu, kutendewa vibaya, hata kifo, lakini alishinda kifo na akapaa Mbinguni, na anatuombea katika mkono wa kulia wa Elohim Baba. Hebu tuwe tayari kumtumikia Yeye kwa kusaidia kuvuta roho zilizo thamani kwa Ufalme Wake wa milele, na kuteseka kwa ajili Yake, hata kifo ikiwa itahitajika.

*******************************

**Somo la Aprili 8, 2023 (Nisan 17, 5783)**

## KUSAMEHEANA

**Somo Kuu: Mathayo. Sura ya 18.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo. 6:15.**

1. Je! Ni nini kinachohitajika kwetu kufanya ili kupokea msamaha wa dhambi zetu? Marko 11:25.

aliyeteuliwa katika Kanisa la Elohim) alitafuta vitu za kumnufaisha na kufuata maisha ya raha? 2 Wakorintho 11:26-28.

12. Je, Paulo aliwatawala watu kwa vitisho, kuwalazimisha na kuwatia hofu, au walikuwa chini ya amri zake kupitia upendo? Matendo 20:31-35.
13. Je, tumeamriwa kufuata mfano uliowekwa naye Paulo, vile vile kufuata nyayo zake Masihi? 1 Wakorintho 11:1.
14. Tunapaswa kutafuta kibali na ushirika wa wale wanaonekana kuwa wakubwa miongoni mwa watu? Warumi 12:16.
15. Ni maelekezo gani mazuri yaliotolewa katika Warumi 12:10?
16. Ni ushuhuda gani tunao katika Waebrania 3:5 kuhusu kiongozi mkuu, aliyechaguliwa na Elohim, katika nyakati za Agano la kale?
17. Ni sifa gani zinazohitajika kwa mtumishi ambazo zimewekwa katika 2 Timotheo 2:24, 25.

******************************

**Somo la Aprili 29, 2023 (Iyar 8, 5783)**

## UMUHIMU WA MAOMBI

**Somo Kuu: Mathayo 7:7-20**
**Fungu La Kukariri: Wafilipi 4:6**

1. Je, ni ahadi gani imewekwa kwa wale huomba na kutafuta vitu wanavyohitaji? Mathayo 7:8.



mwanadamu, zaidi ya hayo tunahakikishiwa kwamba itapita kwa sababu ya kifo na ufufuo wa Yahshua Mwana wa Elohim.

4. Hata katika nyakati za zamani, ni njia gani mbili zilikuwa wazi kwa mwanadamu? Kumb. 30:19; Yer. 21: 8.
5. Je! Yahshua alielezeaje hilo jambo kwa Wayahudi? Yohana 5:40.
6. Ni ujumbe gani wa neema tunapaswa kuwa tunahubiri leo? Ufu. 22:17.

**Maelezo**: Tangia zamani Elohim amekuwa akifikisha neema yake kwa jamii ya wanadamu. Kwa nyakati zote akitekeleza neema yake kwa wanadamu. Tangia zamani wao walikataa rehema na upendo Wake hadi mwisho walimsulubisha Mwana wake mwenyewe. Tunapokaribia kurudi kwa mara ya pili, ndivyo dhabihu aliyoitoa itakataliwa zaidi. Hata hivyo kwa wale wanaomjua, Yeye bado ni yule yule kama alipokuwa hapa duniani.

7. Je! Neema ya Elohim imefunuliwa kwa watu wangapi? Tito 2: 11-15.
8. Ni nini kinachoonyesha upendo usioweza kupimika ambao Masihi anao kwetu sisi? 2 Wakor. 8: 9.
9. Je! Jinsi gani neema imefunuliwa zaidi kwetu sisi? Mstari wa 12.
10. Je! Paulo kwa njia ya unyenyekevu alikiri nini? 1 Wakor.15:10.



2. Je! Elohim atawasamehe wale ambao hawawasamehei wenzao? Mathayo. 6:15; Marko 11:26, Mathayo. 18: 21-22.

**Maelezo**. Elohim haridhiki na huduma ya mdomo au utaratibu tu. Tunapaswa kusamehe kutoka moyoni, na wakati tunapofanya hivyo basi pia tusahau, na tutaacha kuishi ndani ya dhambi ambazo zimesamehewa. Baadhi ya wengine, wakati wanajifanya kusamehe husema: “Ninaweza kusamehe lakini siwezi kusahau”. Wanakuwa na kinyongo.

3. Ni katika hali gani inapaswa mioyo yetu iwe ili tuweze kupata msamaha? Mathayo. 6:12.
4. Je, Elohim alikataza kinyongo? Walawi. 19:18.
5. Je! Agano Jipya linasema nini kuhusu kinyongo? Yakobo 5: 9; Mathayo. 6: 12-24.

**Maelezo**. - Wivu ni dhambi kubwa katika nyakati zote, wakati huu kama vile ilivyokuwa wakati ndugu za Yosefu walipomwonea wivu kwa sababu ya kupendwa na wazazi wake na fadhili za ziada, na pia kwa sababu Elohim alimpenda na kumpa ndoto kuhusu mambo ambayo yangekuja kutimia; kwa hiyo walimtendea vibaya na kumwuza kwa wageni kama mtumwa.

6. Jinsi gani Yusufu mtu wa Elohim aliwasamehe ndugu zake? Mwanzo 45:15.



**Somo la Juni 10, 2023 (Sivan 21, 5783)**

## NYUMBANI YA BAADAYE YA WATAKATIFU

**Somo Kuu: Zaburi 37.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 5: 5.**

1. Dunia hii iliumbwa kwa sababu gani? Isaya 45:18.
2. Je, kuna wakati wowote ambapo ulimwengu huu wote utakuwa ukiwa kabisa? Mwanzo 8:21, 22.
3. Kwa mujibu wa maagizo ya Masihi, tunapaswa kuombaje? Mathayo 6: 9, 10.
4. Watakatifu wataondolewa lini duniani? Mithali 10:30.
5. Mbingu ni ya nani? Zaburi 115: 16.
6. Je, Ibrahimu na mbegu yake walikuwa wamiliki nini kwa ajili ya milki ya milele na milele? Mwanzo 13:14, 15; 17: 8.
7. Je, watakatifu wa kale walipokea ahadi hii? Waebrania 11: 8-13.
8. Ni ahadi gani zilizopo kwa wapole? Mathayo 5: 5.
9. Tutaweza kufarijiwa na nini? Yohana 14: 1-3.
10. Kulingana na Paulo tunatarajia kwenda kwenye makao haya, au tunatarajia Jiji kuja kwetu? Waebrania 13:14; Mathayo 6:10

12. Ni nani tu atapokea hitaji kamili la Elohim? Ufunuo 14:12.

*******************************

**Somo la Mei 13, 2023 (Iyar 22, 5783)**

## NEEMA – ZAWADI KUU YA ELOHIM

**Somo Kuu: Warumi 5: 1-21.**
**Fungu La Kukariri: Waroma 5:21.**

1. Je! Ni tendo gani la kwanza limenakiliwa la neema kwa ajili ya mtu aliyeanguka? Mwanzo 3:21.

   **Maelezo**: Uovu wa dhambi na matokeo yake; kifo kwa pande isiyo na hatia, imeelezewa katika aya hii fupi. Damu isiyo na hatia ilimwagika hili mtu aweze kupata mavazi ya mwili. Hivyo basi aina ya kwanza iliundwa katika Agano la Kale. Ililenga damu iliyomwagika ambayo inaweza kumsitiri mtu wa kiroho kama jinsi mahitaji yao ya kwanza yalitimizwa.
2. Jinsi gani tutajua ya kwamba Abili alipewa maagizo kuhusu mpango wa wokovu? Mwanzo 4: 4.
3. Uhusiano kati ya dhambi na neema ni nini? Warumi 5: 17-20.

   **Maelezo**: Kwa hakika kama jinsi dhambi na mauti zilikuja kupitia kuanguka kwa



2. Jinsi gani Bwana anaonyesha utayari wa Mbinguni kuwapa kwa neema wale huomba? Mathayo 7:11.
3. Kwa nini ni muhimu kuomba Baba yetu wa Mbinguni kwa ajili ya haya mambo yote? Yakobo 1:17.
4. Jinsi gani tunapaswa kuomba? 1 Wakorintho 14:15.
5. Je! Ni nini lazima iambatane na sala ya mtu ili kumpendeza Baba wa Mbinguni? Waebrania 11:6.
6. Ni vipi imani hii inafaa kuwa thabiti? Marko 11:24.
7. Ni nini inafaa ifanywe wakati mtu anapohitaji kuponywa maradhi? Yakobo 5:13-16.
8. Kuna faida na umuhimu, nyakati nyingine, kujificha kabisa mbali, pekee yako ili upate kuomba? Mathayo 6:6.
9. Je, waumini katika nyakati za mitume walikuwa na mikusanyiko kwa ajili ya sala? Matendo 12: 12.
10. Ni mara ngapi Mitume walishawishi Kanisa kuomba? Waefeso 6:18; 1 Wathesalonike 5:17.
11. Ni kwa nini maombi ni muhimu sana? Yohana 15:7.
12. Wakati tunapojikuta katika uwepo wa wale ambao hupinga au kukejeli maombi, au hata kama tutakatazwa kuomba, tutaacha ibada zetu za kawaida? Danieli 6:10.



1. Je, maandiko yanasema nini juu ya matokeo ya mafunzo ya Yezebeli? Ufu. 2: 20-22.
2. Kuna wale ambao wataamka kwa ukweli kwamba walimsaliti Yeye ambaye angeleta uzima wa milele. Je, watatarajia matokeo gani? Mathayo. 27: 3-5.
3. Kwa njia gani Bwana Yahshua aliwatenganisha watu wa kizazi chake na wale wa Yona? Luka 11:32.
4. Je, nini itakuwa hatima ya kusikitisha sana ya wanawali wapumbavu? Mathayo. 25:10, 12.
5. Je, ni jambo gani la kusikitisha wakati Esau alipokuwa akitaka kutubu? Heb. 12: 15-17.
6. Ni sababu gani Bwana hupeana kuhusu wale wasiomtafuta na kuwa wataharibiwa? Mithali. 1: 28-32.
7. Waumini wa uongo watakutana na nini? Mathayo. 7: 21-23.
8. Kwa nini mukuyu fulani ulipaswa kukatwa? Luka 13: 6-9.

   **Maelezo**. - Ingawa mti huu ulikuwa na uwezo wa kuzaa matunda na ulikuwa umepandwa vizuri na kutunzwa na ukafikia umri wa kuzaa matunda, ulikuwa tasa. Haukuwa na nafasi katika bustani ya Bwana. Kila mmoja anapaswa kujichunguza mwenyewe, na kutoa hesabu ya maisha yake ili kuona kama yeye ana thamani yoyote kwa Bwana katika kuvuta roho za watu.

*******************************



7. Katika kukabiliana na waliokosa, ni hisia gani tunapaswa kuwa nazo? Mathayo. 18:33.
8. Je! Ni nini watatarajia wale ambao hawawezi kuonyesha huruma kwa wengine? Yakobo 2:13.
9. Katika mfano wa Mathayo 18, nini kilichotokea kwa mtumishi aliyepaswa kulipa deni kubwa? Mathayo. 18: 23-27.
10. Baadaye wakati mtu aliyekuja, ambaye alipaswa kulipa deni ndogo sana la huyo mtu, ni huruma gani alipokea? Mathayo. 18: 28-30.
11. Je! Mtumishi asiye na huruma alipokea nini kutoka kwa Bwana wake? Mathayo. 18: 32-35.
12. Je, haya yote yameandikwa kwa nani? 1 Wakor. 10:11; Warumi. 15: 4; 2 Tim. 3:16, 17.

*******************************

**Somo la Aprili 15, 2023 (Nisan 24, 5783)**

## KUFUATA NYAYO ZAKE

**Somo Kuu: Wafilipi 2:1-18.**
**Fungu la Kukariri: Wafilipi 2:5.**

1. Je! Ni nia gani inapaswa kuwa ndani yetu kuhusu wokovu wa wanadamu wenzetu? Wafilipi 2:4,5.
2. Je! Mwokozi wetu alitoa onyo gani kuhusu kutamani? Luka 12:15.

**Maelezo**: Maombi ni njia ya kuwasiliana na mbinguni na kumkaribia Baba yetu wa Mbinguni. Mhudumu katika wakati mmoja alisema: “Sina hofu kwa ajili ya mvulana au msichana, mwanaume au mwanamke, ambaye huomba kwa dhati mara tatu kwa siku.”

*******************************

**Somo la Mei 6, 2023 (Iyar 15, 5783)**

## IMANI - HITAJI LA MAISHA YA UTAUWA

**Somo Kuu: 2 Wakorintho 4**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 4:2**

1. Ili kumpendeza Elohim, tunafaa kumiliki nini? Waebrania 11:6.
2. Ni wapi ambapo kulikuwa na tendo la kwanza la imani katika upatanisho wa damu? Waebrania 11:4.
3. Ni kitendo gani cha imani kilihitajika jioni ya Pasaka? Kutoka 12:7.

**Maelezo**: Kuwaua kondoo wa Pasaka ilikuwa haitoshi. Ilibidi kila mmoja kujua kama damu imepakwa kwa miimo ya nyumba. Haitoshi leo kwa kujua kwamba Masihi aliishi na kufa, kwani kila mtu lazima ajitoe mwenyewe kwa dhabihu aliyoifanya kwa ajili yetu.



4. Katika siku zilizopita, kwa nini neno halikuwa na faida kwa wana wa Israeli? Waebrania 4:2.
5. Jinsi gani Mwisraeli alionyesha imani katika upatanisho kwa umwagaji wa damu? Mambo ya Walawi 4:27-30.
6. Katika maelezo yaliyotolewa katika Biblia, imani ni nini? Waebrania 11:1
7. Ni wangapi wanayoimiliki imani hii? Warumi 12:3.
8. Jinsi gani wengi hujidai, ambayo inaonyesha ukosefu wa imani ndani yao? Yohana 6:30.
9. Kabla ya kuuona utukufu wa Elohim, tunapaswa kufanya nini? Yohana 11:40.

**Maelezo**: Yahshua angeweza kusema neno na jiwe lingeondoka chini ya udhibiti wa Elohim, lakini alichagua kutumia nguvu za kibinadamu kama inavyowezekana. Kwa ombi lake katika Yohana 11:39, ilionekana ukosefu wa imani katika moyo wa Martha. Baada ya nguvu za kibinadamu kufika kikomo chake, katika Yohana 11:41, Alitoa wito kwa Baba wa kufanya kile uwezo wa binadamu haukuweza kufanya; kufufua maiti. Tukiongea kwa kiroho, Elohim pekee yake anaweza kutufufua kutoka kifo cha kiroho na uozo.

10. Kwa nini Yahshua alimpongeza huyo ofisa kupita wengine? Mathayo. 8:5-8.
11. Ni nini hutuongoza kuamini kwamba Masihi atarudi hivi karibuni? Luka 18:8.



**Maelezo**. Ni dhahiri jinsi gani kwamba njia za ulimwengu huu wa sasa ziko kinyume na njia za mbinguni. Hatupaswi kuipenda dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. 1 Yohana 2:15. Pesa hupima hadhi na umaarufu wa mtu leo katika kila sehemu ya dunia. Ukuu wake unazingatiwa karibu kote ulimwenguni na kile anachomiliki. Shetani alimtolea Mwokozi wetu falme za ulimwengu huu, kama angemtumikia, lakini alikataa toleo hilo. Watumishi wake wanapaswa kufanya vivyo hivyo, na kuweka hazina mbinguni, na si duniani.

3. Je, tunapaswa kutafuta kuenenda kulingana na mwili au kwa uwepo wa Roho? Warumi 8:4,5.
4. Je! Ni nini imesemwa juu ya hali zenye kutatanisha za mioyo ya wanadamu, kabla tu ya kurudi kwa Masihi? Luka 21:24-26.

**Maelezo**. Unabii huu ulitimizwa kwa namna ya ajabu, huku Wayahudi wakiwa wametawanyika katika kila sehemu ya dunia, na Yerusalemu ikakanyagwa na Mataifa kwa karibu miaka elfu mbili. Sasa, hata hivyo, tunawaona wakirudi Yerusalemu na Israeli kutoka kila nchi. Wamekusanyika hapo sasa kutoka kwa mataifa, na tunaona dhiki na fadhaa ambayo inaonekana kila mahali kati ya mataifa yote. Mioyo ya wanadamu pia imejawa na hofu, ya mambo yanayokuja kutokea juu ya ulimwengu kama vile



8. Ni mfano gani wa Agano la Kale unaothibitisha hili? 1 Samweli 10:6, 9; 1 Mambo ya Nyakati 10:13.
9. Je, ni kwa muda gani tunapaswa kubaki waaminifu kwa Injili? Ufunuo 2:10.
10. Ni maandalizi gani ya kutosha yamepeanwa kwa wote watakaoanguka katika dhambi? 1 Yohana 2:1, 2 .
11. Je, urejesho utakuwa kamili kwa kiasi gani? Waebrania 7:25.
12. Je, ni nini hatupaswi kamwe kufanya? Waebrania 2:3.
13. Je! Ni mambo gani mawili muhimu yatatuongoza kwenye uzima wa milele? Waebrania 11:27; 12:2.
14. Je! Ni kweli gani ya thamani inayong’aa kama mwanga kwa wote? Yuda 24, 25 .

*******************************

**Somo la Juni 3, 2023 (Sivan 14, 5783)**

## AWAMU YA HUZUNI YA TOBA

**Somo Kuu: 1 Wafalme 21: 1-23; Mithali. 1: 24-31.**
**Fungu La Kukariri: Mithali. 1:28.**

**Maelezo**. - Baba wa mbinguni anatoa nafasi ya kutosha, au nafasi ya toba, lakini wengi hawatasikiliza. Hata hivyo, kuna wakati unakuja ambapo watu wote watapiga magoti mbele yake, lakini, jambo la kusikitisha, wakati utakuwa umeisha.